# TUJIFUNZE BIBLIA

## *SOMO LA 10*

## IBADA YA KIKRISTO

Tangu mwanzo watu wamemwabudu Mungu. Walakini, Mungu hafurahi na ibada ya watu wote. Kwa mfano, Kaini na Habili walikuwa wakimwabudu Mungu walipomtolea sadaka. Lakini, twasoma: "*Bwana akamtakabali Habili na sadaka yake; bali Kaini hakumtakabali, wala sadaka yake.*" (Mwanzo 4:4-5). Mfalme Sauli naye alikuwa akimwabudu Mungu yeye yule. Hata hivyo, Mungu hakupokea sadaka yake (1 Samweli 15:17-26).

Yesu ametuonya kwamba imani haitoshi pasipo kuzitii sheria za Mungu mwenyewe. Maana, alisema:

"*Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni.*" Mathayo 7:21

"*Watu hawa huniheshimu kwa midomo; ila mioyo yao iko mbali nami. Nao waniabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu.*" Mathayo 15:8-9

1. Je! watu wote wanaomwamini Yesu wataingia mbinguni? ____________________
2. Hata ingawa mtu amemwamini Mungu, lakini ibada yake itakuwa bure ikiwa anayafuata mafundisho yaliyo maagizo ya nani? ____________________

Mwanadamu hana ruhusa kumwabudu Mungu jinsi anavyotaka, bali Yesu alisema:

"*Mungu ni Roho, nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli.*" Yohana 4:24

3. Imetupasa kumwabudu Mungu katika nini? ____________________na ____________________

Kumwabudu Mungu katika kweli maana yake ni kushika neno lake. Maana, Yesu alituombea akasema.

"(Mungu) *Uwatakase kwa ile kweli; neno lako ndiyo kweli.*" Yohana 17:17

4. Je! twaweza kujifunza kumwabudu Mungu katika kweli kwa kusoma maneno ya watu au maneno ya Mungu? ____________________

Basi, imetupasa kuchunguza sana Biblia kusudi tuhakikishe kwamba tunamwabudu Mungu jinsi anavyotaka Yeye.

Katika agano la kale Mungu aliwaamuru Wayahudi wajenge nyumba iliyoitwa hekalu. Nyumba hiyo ilikuwa mahali pa kumwabudia Mungu. Tena, Mungu aliwateua Haruni na watoto wake kuwa makuhani wenye kutoa dhabihu na sadaka. Mambo hayo ya kimwili yalikuwa kama mfano au kivuli cha mambo ya kiroho ya kikristo (Waebrania 8:1-5; 9:23-24). Wakristo hawana haja ya kujenga hekalu la matofali, maana twasoma:

"*Mungu aliyeufanya ulimwengu na vitu vyote vilivyomo, yeye, kwa kuwa ni Bwana wa mbingu na nchi, hakai katika hekalu zilizojengwa kwa mikono.*" Matendo 17:24

"*Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu? Kama mtu akiliharibu hekalu la Mungu, Mungu atamharibu mtu huyo. Kwa maana hekalu la Mungu ni takatifu, ambalo ndilo ninyi.*" 1 Wakorintho 3:16-17

5. Mungu hakai katika nyumba zilizojengwa na nini? ___________________

6. Wakristo wenyewe wamekuwa hekalu la Mungų. Je! ni nani anayekaa ndani yao?

___________________

Wala si kwamba Wakristo ni hekalu tu bali kila Mkristo ni kuhani pia. Twasoma:

"*Ninyi nanyi, kama mawe yaliyo hai, mmejengwa mwe nyumba ya Roho, ukuhani mtakatifu, mtoe dhabihu za roho, zinazokubaliwa na Mungu, kwa njia ya Yesu Kristo.*" 1 Petro 2:5

7. Wakristo wote ni makuhani wanaotoa dhabihu gani? ___________________

Wakristo hawana haja ya kumtolea Mungu dhabihu za wanyama kama Wayahudi walivyofanya bali twasoma:

"*Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana.*" Warumi 12:1

8. Wakristo wote ni makuhani wanaojitoa miili yao kuwa nini? ___________________

Mistari mingine ya Biblia inayotuambia kuhusu sadaka na dhabihu za kikristo inasema:

"*Basi, kwa njia yake yeye (Yesu), na tumpe Mungu dhabihu ya sifa daima, yaani, tunda la midomo iliungamayo jina lake. Lakini msisahau kutenda mema na kushirikiana; maana sadaka kama hizi ndizo zimpendezazo Mungu.*" Waebrania 13:15-16

9. Wakristo wameambiwa kumpa Mungu dhabihu gani? ___________________

10. Wakristo wote ni makuhani wanaotoa sadaka gani? ___________________ na___________________

Baadhi ya watu hudhani kwamba mtu ye yote aendaye kusali kanisani atakubaliwa na Mungu. Walakini Biblia yasema:

"*Mtu akidhani ya kuwa anayo dini, wala hauzuii ulimi wake kwa hatamu, hali akijidanganya moyo wake, dini yake mtu huyo haifai. Dini iliyo safi, isiyo na taka mbele za Mungu Baba ni hii, Kwenda kuwatazama yatima na wajane katika dhiki yao, na kujilinda na dunia pasipo mawaa.*" Yakobo 1:26-27

11. Je! ibada au dini iliyo safi ni kuhudhuria kanisani tu au ni kufanywa mema siku zote pia?

___________________

Basi, inatakiwa kwa Wakristo wamwabudu Mungu katika matendo yao yote, lakini wameamriwa kukusanyika pamoja pia. Twasoma:

"*Wala tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine; bali tuonyane; na kuzidi kufanya hivyo, kwa kadiri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia. Maana, kama tukifanya dhambi kusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi; bali kuna kuitazamia hukumu kwenye kutisha, na ukali wa moto ulio tayari kuwala wao wapingao.*" Waebrania 10:25-27

12. Wakristo wasiache kufanya nini? ____________________

13. Mkristo ambaye anatenda dhambi kwa kusudi (kwa mfano, kuacha kukusanyika) amebaki kuitazamia hukumu gani? ____________________

Wakristo wanapokusanyika pamoja kuna mambo fulani yatakiwayo yatendeke. Mambo hayo. ni: **(1)** kuomba, **(2)** kuimba, **(3)** kuhubiri neno la Mungu, **(4)** kutoa changizo, na **(5)** kula chakula cha Bwana. Ebu! tuyachunguze mambo hayo moja moja katika Biblia.

## KUOMBA NA KUSHUKURU

"*Msijisumbue kwa neno lo lote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu.*" Wafilipi 4:6

Paulo alisema: "*Basi, kabla ya mambo yote, nataka dua, na sala, na maombezi, na shukrani, zifanyike kwaajili ya watu wote; kwaajili ya wafalme na wote wenye mamlaka tuishi maisha, ya utulivu na amani, katika utauwa wote na ustahivu.*" 1 Timotheo 2:1-2

14. Tutoe dua, na sala, na maombezi pamoja na nini? ____________________

## KUIMBA

Paulo alisema: "*Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote, mkifundishana na kuonyana kwa zaburi, na nyimbo, na tenzi za rohoni; huku mkimwimbia Mungu kwa neema mioyoni mwenu.*" Wakolosai 3:16

15. Wakristo wafundishane na kuonyana kwa njia gani?
____________________, ____________________na____________________

16. Tumwimbie Mungu kwa neema katika nini? ____________________

Baadhi ya watu walioishi chini ya Agano la Kale waliwahi kutumia zeze au vyombo vya muziki wakimwimbia Mungu. Walakini, katika somo la nne tulijifunza kwamba, Wakristo hawapo chini ya Agano la Kale bali Agano Jipya (Waebrania 8:13; 9:15; 10:9; Warumi 7:6; Wagalatia 3:23-25; 5:4). Hakuna hata mstari mmoja katika Agano Jipya ambao unaturuhusu kutumia vyombo vya muziki katika kumwimbia Mungu. Wala hakuna mstari mmoja unaotufundisha kuweka kwaya, bali Biblia imesema "*mkifundishana na kuonyana kwa zaburi, na nyimbo, na tenzi za rohoni*" (Wakolosai 3:16). Imetupasa

kukumbuka hatari ya kuongeza au kuondoa neno lo lote katika mpango wa Mungu (Wagalatia 1:8; Mathayo 15:8-9; Ufunuo 22:18-19).

## KUHUBIRI NENO

Paulo alisema: "*Lihubiri neno, uwe tayari,wakati ukufaao na wakati usiokufaa, karipia, kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho. Maana utakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima; ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia waalimu makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti; nao watajiepusha wasisikie yaliyo kweli, na, kuzigeukia hadithi za uongo… Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine.*" 2 Timotheo 4:2-4; 2:2

17. Timotheo alionywa kulihubiri neno la Mungu kwa sababu baadhi ya Wakristo watajipatia waalimu wa uongo wakifuata nia zao wenyewe na kujiepusha wasisikie nini?

____________________

## KUTOA

Mungu anataka Wakristo wapendane na kusaidiana. Yesu alituonya kuhusu hatari ya kujiwekea utajiri wa kimwili badala ya utajiri wa kiroho. Alisema:

"*Msijiwekee hazina duniani, nondo na kutu viharibupo, na wevi huvunja na kuiba; bali jiwekeeni hazina mbinguni, kusikoharibika kitu kwa nondo wala kutu, wala wevi hawavunji wala hawaibi; kwa kuwa hazina yako ilipo, ndipo utakapokuwapo na moyo wako.*" Mathayo 6:19-21

"*Hapo atakapokuja Mwana wa Adamu katika utukufu wake, na malaika watakatifu wote pamoja naye, ndipo atakapoketi katika kiti cha utukufu wake; … Kisha atawaambia na wale walioko mkono wake wa kushoto, Ondokeni kwangu, mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele, aliowekewa tayari Ibilisi na malaika zake; kwa maana nalikuwa na njaa, msinipe chakula; nalikuwa na kiu, msininyweshe; nalikuwa mgeni, msinikaribishe; nalikuwa uchi, msinivike; nalikuwa mgonjwa, na kifungoni, msije kunitazama. Ndipo hao pia watajibu, wakisema, Bwana, ni lini tulipokuona wewe una njaa, au una kiu, au u mgeni, au u uchi, au u mgonjwa, au u kifungoni, tusikuhudumie? Naye atawajibu, akisema, Amin, nawaambia, Kadiri msivyomtendea mmojawapo wa hao walio wadogo, hamkunitendea mimi.*" Mathayo 25:31, 41-45

18. Mkristo amnyimaye mwenzake amemnyima nani pia? ____________________

Wayahudi walipewa amri ya, kumtolea Mungu zaka (yaani, sehemu ya kumi ya mali yao). Basi Mungu aliwakemea Wayahudi akisema:

"*Je! mwanadamu atamwibia Mungu? lakini ninyi mnaniibia mimi. Lakini ninyi mwasema, Tumekuibia kwa namna gani? Mmeniibia zaka na dhabihu. Ninyi mmelaaniwa kwa laana; maana mnaniibia mimi, naam, taifa hili lote. Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba yangu, mkanijaribu kwa njia hiyo, asema Bwana wa majeshi; mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha, au la.*" Malaki 3:8-10

19. Wayahudi walimwibia Mungu wakimnyima nini? ____________________

Wakristo hawajapewa amri ya kutoa zaka. Walakini, haina maana kwamba Mungu atafurahi na Mkristo ambaye anamnyima. Ebu! tuone mistari mingine inayohusu kutoa.

"*Lakini nasema neno hili, Apandaye haba atavuna haba; apandaye kwa ukarimu atavuna kwa ukarimu. Kila mtu na atende kama alivyokusudia moyoni mwake, si kwa huzuni, wala si kwa lazima; maana Mungu humpenda yeye atoaye kwa moyo wa ukunjufu. Na Mungu aweza kuwajaza kila neema kwa wingi, ili ninyi, mkiwa na riziki za kila namna sikuzote, mpatekuzidi sana katika kila tendo jema.*"

2 Wakorintho 9:6-8

20. Mungu humpenda nani? ____________________

Wakristo wameambiwa kutoa changizo kwa kadiri wanavyofanikiwa. Twasoma:

"*Kwa habari ya ile changizo kwa ajili ya watakatifu, kama vile nilivyoamuru makanisa ya Galatia, nanyi fanyeni vivyo. Siku ya kwanza ya juma kila mtu kwenu na aweke akiba kwake, kwa kadiri ya kufanikiwa kwake; ili kwamba michango isifanyike hapo nitakapokuja.*" 1 Wakorintho 16:1-2

21. Wakristo wa mji wa Korintho waliambiwa kutoa changizo katika siku gani?

____________________

22. Kila mtu aliambiwa kutoa kwa kadiri gani? ____________________

Mungu anajua hali zetu na kufanikiwa kwetu. Mkristo akijaribu kudanganya akisema ametoa kwa kadiri ya kufanikiwa kwake hali sivyo, basi, yuko katika hatari. Maana, katika Matendo 5:1-11 twasikia habari ya Wakristo wawili waliouawa na Mungu kwa sababu walitaka kudanganya katika kutoa!

Hapo juu tumeona jinsi changizo inavyotolewa kwa ajili ya kuwasaidia wanyonge. Lakini, sababu ya pili ya kutoa ni kuwasaidia watu wanaohubiri neno la Mungu. Paulo alisema:

"*Ikiwa sisi tuliwapandia ninyi vitu vya rohoni, je! ni neno kubwa tukivuna vitu vyenu vya mwilini?... Na Bwana vivyo hivyo ameamuru kwamba wale waihubirio Injili wapate riziki kwa hiyo Injili.*"

1 Wakorintho 9:11,14

"*Mwanafunzi na amshirikishe mkufunzi* (yaani, mwalimu) *wake katika mema yote.*" Wagalatia 6:6

23. Je! mhubiri anaweza kulishwa na kanisa? ____________________

## CHAKULA CHA BWANA

Yesu aliwaamuru wanafunzi wake wale mkate na wanywe kikombe chake kuwa kumbukumbu la mauti yake. Twasoma:

"*Nao walipokuwa wakila, Yesu alitwaa mkate, akabariki, akaumega, akawapa wanafunzi wake, akasema, Twaeni, mle; huu ndio mwili wangu. Akakitwaa kikombe, akashukuru, akawapa, akisema, Nyweni nyote*

*katika hiki; kwa maana hii ndiyo damu yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi.*” Mathayo 26:26-28

24. Je! baada ya kuwapa wanafunzi mkate, Yesu aliwaamuru kwamba wote wanywe kikombe chake au baadhi yao tu? ____________________

Wako watu leo wanaowanyima wenzao kikombe cha Bwana wakiwapa mkate tu. Watu hao husema kwamba mwili hautakosa kuwa na damu ndani yake na, kwa hiyo, Mkristo akipata mkate (ulio mfano wa mwili) atakuwa amepata damu pia. Yesu alijua kwamba mwili una damu ndani yake. Walakini, Yesu aliwaeleza wanafunzi kwamba damu yake haitakaa mwilini mwake bali itamwagika. Basi, ndiyo maana alisema “nyweni nyote.” Tena twasoma:

“*Basi Yesu akawaambia, Amin, amin, nawaambieni, Msipoula mwili wake Mwana wa Adamu na kuinywa damu yake, hamna uzima* ndani yenu. *Aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu anao uzima wa milele; nami nitamfufua siku ya mwisho.*” Yohana 6:53-54

25. Yesu alisema kwamba hatutakuwa na uzima ndani yetu tusipokula mwili wake na kuinywa nini? ____________________

Biblia haijawaamuru Wakristo watoe fedha wala kuungama dhambi kwa padiri kusudi wapate chakula cha Bwana. Wala hakuna mahali katika Biblia panaposema kwamba mtu apate kwanza Kipaimara. Hata neno “Kipaimara” haimo katika Biblia.

Madhehebu fulani humweka mtu katika kanisa ambaye wanamwita padiri. Kisha wanasema kwamba padiri huyo ni kuhani ambaye peke yake ameruhusiwa kushika chakula cha Bwana. Tena, watu hawa hujenga meza ambayo wanaiita “dhabahu” (yaani, mahali pa kutoa dhabihu na sadaka). Kisha wasema kwamba wakati padiri anapoweka chakula cha Bwana juu ya meza hiyo, basi kinageuzwa kuwa mwili halisi wa Yesu. Hivyo wanadhani kwamba kuhani (yaani, padiri) ameutoa mwili wake Yesu uwe dhabihu tena. Walakini, Biblia hupinga mafundisho hayo. Ebu, tuone.

Jambo la kwanza, katika Biblia huwezi kusoma habari ya padiri bali kila Mkristo ni kuhani mbele ya Mungu (1 Petro 2:5,9: Ufunuo 1:6).

Jambo la pili; Wakristo hawajaambiwa kujenga dhabahu wala kuutoa mwili wa Yesu uwe dhabihu. La! bali Wakristo wote wameamriwa kujitoa miili yao wenyewe kwa Mungu kuwa “dhabihu iliyo hai” (Warumi 12:1-2; Waebrania 13:15-16).

Jambo la tatu, ingawa makuhani ni wengi walakini kuhani mkuu ni mmoja tu. Wala makuhani wote hawakuruhusiwa kutoa dhabıhu kwa ajili ya ondoleo la dhambi bali kuhani mkuu peke yake. Basi, Yesu ni kuhani mkuu wa Wakristo ambaye amekwisha kutoa dhabihu kwa ajili ya dhambi. Tena, Biblia inasema waziwazi kwamba hatuna haja kwa mwili wa Yesu kuzidi kutolewa, bali Yesu alijitoa mara moja tu. Twasoma:

“*Kristo aliingia mbinguni hasa, aonekane sasa usoni pa Mungu kwa ajili yetu; wala si kwamba ajitoe mara nyingi, kama vile kuhani mkuu aingiavyo katika patakatifu kila mwaka kwa damu isiyo yake; kama ni hivyo, ingalimpasa kuteswa mara nyingi tangu kuwekwa msingi wa ulimwengu; lakini sasa, mara moja*

*tu, katika utimilifu wa nyakati, amefunuliwa, azitangue dhambi kwa dhabihu ya nafsi yake.*”

Waebrania 9:24-26

26. Je! Wakristo wanapokula chakula cha Bwana wanamtoa Yesu awe dhabihu tena?

___________________

Basi, chakula cha Bwana hakigeuzwi kuwa mwili halisi wa Yesu bali ni ukumbusho au mfano tu. Ebu! tuhakikishe jambo hili.

“*Kwa maana mimi nalipokea kwa Bwana niliyowapa nanyi, ya kuwa Bwana Yesu usiku ule aliotolewa alitwaa mkate, naye akiisha kushukuru akaumega, akasema, Huu ndio mwili wangu ulio kwa ajili yenu; fanyeni hivi <u>kwa ukumbusho</u> wangu. Na vivi hivi baada ya kula akakitwaa kikombe, akasema, Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu; fanyeni hivi kila mnywapo, kwa ukumbusho wangu. Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, <u>mwaitangaza</u> mauti ya Bwana hata ajapo.*”

1 Wakorintho 11:23-26

27. Yesu aliwaamuru wanafunzi wake wale mkate ambao ulikuwa mfano au ukumbusho wa nini?

___________________

28. Kikombe chake Yesu ni ukumbusho wa nini? ___________________

29. Tunapokula chakula cha Bwana je! tunamtoa tena awe sadaka au tunatangaza kwamba alikufa?

___________________

Kama tulivyosoma, Wakristo hutangaza mauti ya Bwana wanapokula chakula chake. Basi, <u>Yesu alifufuka katika wafu siku ya kwanza</u> ya juma (Luka 24:1-8). Ndiyo maana inatakiwa kwa Wakristo wale chakula cha Bwana <u>katika siku ya kwanza</u> ya kila juma kusudi watangaze kufa na kufufuka kwake. Ndivyo Wakristo walivyofanya katika siku za mitume. Twasoma:

“*Hata siku ya kwanza ya juma, tulipokuwa tumekutana ili kumega mkate, Paulo akawahutubu, akiazimu kusafiri siku ya pili yake, naye akafuliza maneno yake hata usiku wa manane.*” Matendo 20:7

Siku ya kukusanyika pamoja kumega chakula cha Bwana ni siku gani?

Siku ya kwanza ya juma si sawa na sabato. Wayahudi waliamriwa kuishika Sabato ambayo ilikuwa siku ya saba (Kutoka 31:16-17). Walakini, Mungu amekomesha Sabato (Hosea 2:11; Wakolosai 2:16). Wakristo hawajaamriwa kuishika sabato bali siku ya kwanza ya juma. Kwa bahati mbaya, kalenda ya kiswahili imepatikana kwa Waarabu ambao hawahesabu siku kama Wayahudi na Wakristo. Kwa hiyo, katika kiswahili siku ya kwanza ya juma huitwa “Jumapili.” Basi, Jumapili ni siku ya kwanza ya juma.

Hata ingawa siku ya kwanza ya juma ni siku maalum ya kupata chakula cha Bwana na ya kutoa changizo (1 Wakorintho 16:1-2), walakini haina maana kwamba ndiyo siku pekee ambayo Wakristo wanaweza kukusanyika kumwabudu Mungu. La! bali Biblia inatuambia kwamba watu wale waliobatizwa huko Yerusalemu katika siku ya Pentekoste walijitoa sana katika kukusanyika. Wengi wao walikuwa wakisali pamoja kila siku (Matendo 2:46). Basi, tusichoke katika kukusanyika! Amri hiyo imetolewa na Mungu kwa faida yetu tupate kujengana.

**********************************************************************************

Jina lako …………………………………………………
Anwani yako ……………………………………………

***KANISA la KRISTO***

***Tanzania***